SHIRIKA LA RELI TANZANIA

# RELI na MATUKIO
Gazeti
Oktoba 08, 2021



Gazeti la Reli | Toleo Namba 17 | Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

# MRADI WA SGR WAPAMBA MOTO, TRENI YATEMBEA KUTOKA PUGU HADI KILOSA



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akishuka katika treni ya uhandisi ya mkandarasi Yapi Merkezi alipowasili kituo cha kupanga treni za mizigo na Karakana eneo la Kwala mkoani Pwani wakati wa ziara kukagua mradi wa SGR Dar es Salaam - Kilosa, Septemba 2021.

Na Mwandishi wetu

Kipande cha reli kutoka Pugu Dar es Salaam hadi Kilosa mkoani Morogoro chakamilika ambapo Waziri Mkuu wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa ametembelea kipande hiko cha mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR chenye urefu wa kilometa 245 na kutumia treni ya uhandisi ya mkandarasi kukagua mradi huo, Septemba 12 2021.

Waziri Mkuu amesema kuwa ziara hiyo imelenga kukagua njia ya reli hiyo kama ipo salama na imekamilika na pia kuhakikisha kuwa vituo vyote vilivyojengwa kwaajili ya abiria vimekamilika.

“Treni inayokuja itakuwa inasukumwa kwa umeme na nimejihakikishia uwepo wa nguzo kutoka huko na zimewekwa na nyaya“ alisema Mhe. Majaliwa.

Mhe. Majaliwa ameeleza kuwa reli hiyo ya SGR itawekwa uzio kwa ajili ya usalama wa binadamu, mifugo na wanyama kwa kuwa treni hiyo itakuwa na kasi kubwa na haitaruhusiwa kwa mtu yeyote kukatiza ama kukaa karibu na eneo la reli ili kuepusha ajali zinazoweza kutokea.

Inaendelea Uk. 2



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC Prof. John Kondoro (wa pili kulia) akipokea zawadi ya asali kutoka kwa mkuu wa mkoa wa Tabora Dkt. Batilda Buriani kama ishara ya kuonesha mazao yanayopatikana Tabora na kuzitangaza, katika ukumbi wa mikutano uliopo ofisi ya mkuu wa mkoa, Septemba 2021.

# MRADI WA SGR WAPAMBA MOTO, TRENI YATEMBEA KUTOKA PUGU HADI KILOSA



Inatoka Uk. 1



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (kushoto) akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (kulia) alipokuwa njiani kuelekea Kilosa mkoani Morogoro akitokea Dar es Salaam kwa kutumia treni ya uhandisi, Septemba 2021.

Aidha, Waziri Mkuu amesema kuwa vituo vyote vya stesheni vya awamu ya kwanza Dar es Salaam - Morogoro vimekamilika kuanzia cha Dar es Salaam, Pugu, Soga, Ruvu, Ngerengere na Morogoro lakini pia kwa kipande cha pili Stesheni ya Mkata na Kilosa nazo zimekamilika

“Nimekagua jengo la abiria Dar es Salaam lijulikanalo kama Tanzanite, limekamilika kwa asilimia 100 “ alisema Mhe. Majaliwa.

Mhe. Majaliwa amesema kuwa wananchi wakae tayari kupokea behewa za treni za SGR ambazo zinatarijia kuwasili nchini mnamo mwezi Novemba na kuanza kufanyiwa majaribio katika njia ya reli

Mhe. Majaliwa amewataka wananchi kutumia fursa za mradi huo kwa kuanzisha nyumba za wageni pamoja na biashara mbalimbali ili kuzidi kujipatia kipato ili uchumi wa nchi uweze kuendelea kukua kwa kasi.

Waziri Mkuu ametembelea maeneo mbalimbali zikiwemo stesheni za SGR, kituo cha treni za mizigo na karakana eneo la Kwala mkoani Pwani, pia amekagua reli, nguzo za umeme pamoja na mitambo ya umeme.

Aliyekuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Leonard Chamuriho amesema kazi inayofanyika ni kubwa sana katika kutekeleza mradi huo wa kimkakati wenye urefu wa kilometa 1219 kutoka Dar es Salaam - Mwanza ambapo kipande cha Dar es Salaam - Morogoro tayari kimekamilika kwa asilimia 93 na Morogoro – Makutupora kikikamilika kwa asilimia 70.

“Mhe. Waziri Mkuu ametembelea na kukagua mradi kipande hiki cha kwanza na amejionea mwenyewe maendeleo makubwa yaliyofanyika” alisema Mhe.Chamuriho.

Inaendelea Uk. 3

# MRADI WA SGR WAPAMBA MOTO, TRENI YATEMBEA KUTOKA PUGU HADI KILOSA

Inatoka Uk. 2

Vilevile, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa ameeleza kuwa mahandaki yote yamekamilika kwa asilimia 100, pia madaraja makubwa 51 ambayo yamekamilika kwa zaidi ya asilimia 70 pamoja na makalavati 622.

Pia Ndugu Kadogosa ameongeza kuwa njia zote zenye vivuko vya binadamu na wanyama pamoja na magari zimetengwa ili kuepusha njia ya reli isiwe na uhusiano na shughuli nyingine za kibinadamu kwa sababu za kiusalama.

## Matukio katika Picha;



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akisaini kitabu cha wageni alipowasili katika stesheni ya SGR Kilosa mkoani Morogoro akitokea Dar es Salaam kwa kutumia treni ya uhandisi ya mkandarasi wa SGR, Septemba 2021.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (kulia) akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (kushoto) kuhusu jengo la Stesheni ya SGR Kilosa mkoani Morogoro, Septemba 2021.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (kulia) akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (kushoto) kuhusu ujenzi wa madaraja ya reli ya kisasa - SGR Kilosa mkoani Morogoro, Septemba 2021.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa (kulia) akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (kushoto) kuhusu jengo la Stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam, Septemba 2021.

# BENKI YA BIASHARA TANZANIA WATEMBELEA UJENZI WA SGR DAR – MWANZA

Na Mwandishi wetu




Meneja Mradi wa Ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Mwanza - Isaka Mhandisi Machibya Masanja akiwaonesha ramani ya eneo la ujenzi wa reli ya Kisasa Mwanza hadi Isaka timu ya wawakilishi kutoka Benki ya Biashara Tanzania katika kambi ya Malampaka mkoani Simiyu, Septemba 2021.

Timu kutoka Benki ya Biashara Tanzania - TCB, ikiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo Ndugu Sabasaba Moshingi imetembelea mradi wa ujenzi wa reli ya Kisasa - SGR kuanzia jengo la stesheni ya SGR Dar es salaam hadi Mwanza, Septemba 2021.

Katika ziara hiyo iliyolenga kutazama maendeleo ya kazi na fursa za uwekezaji katika awamu ya kwanza ya mradi wa SGR Dar es Salaam – Mwanza, timu kutoka TCB imetembelea stesheni za Dar es Salaam, Soga na Morogoro sambamba na karakana ya treni za kisasa, katika kipande cha kwanza cha mradi, huku katika kipande cha pili cha mradi wakitembelea stesheni ya Kilosa, handaki namba mbili la SGR, jengo la makao makuu ya TRC na stesheni ya Dodoma.

Kwa upande wa kipande cha tano cha Mwanza – Isaka, timu hiyo ilitembelea ujenzi wa kambi ya Malampaka mkoani Simiyu na Fela mkoani Mwanza.

Akiukaribisha ugeni huo katika eneo la ujenzi wa stesheni ya SGR na Makao Makuu ya Shirika la Reli Tanzania jijini Dodoma, Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa ameeleza kuwa TCB ni wadau muhimu kwa Shirika la Reli Tanzania na kuwa ziara hiyo itaimarisha zaidi uhusiano kati ya taasisi hizo mbili za umma.

“Tunawashukuru sana wenzetu TCB kwa kututembelea wakiwa kama wadau wetu wa kifedha, wanapokuja kuona tunachokifanya inasaidia wao kufahamu zaidi uhalisia wa kazi inayofanyika” alisema Kadogosa.

Kadogosa aliongeza kuwa ziara hiyo ni chachu ya uwekezaji kupitia majengo mbalimbali yaliyopo katika mradi wa SGR ambayo ni fursa mpya za kiuchumi kwa taasisi na mtanzania mmoja mmoja.

“Lakini pia kupitia ziara hii, tunawapitisha kuziona fursa katika maeneo yetu na majengo yaliyopo kwenye mradi ili kuwekeza” alisema Mkurugenzi Mkuu, Kadogosa.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa TCB, Sabasaba Moshingi ameeleza kuwa ziara hiyo katika mradi wa SGR ni hatua muhimu katika historia ya uhusiano kati ya TCB na TRC na Kuwa wanaamini kwamba kukamilika kwa reli ya Kisasa kutapelekea mabadliko makubwa kwa taifa.

“Dira yetu ni kuhakikisha kuwa tunawasaidia watanzania kupata mikopo, huduma za kibenki na kuwasaidia kufikia malengo yao, kupitia mradi huu, serikali imeonesha kuwa sekta ya umma inaweza kufanya mambo makubwa kwahiyo ushirikiano wetu utasaidia TRC kufikia malengo yake huku TCB kama mdau ikinufaika na matokeo hayo pia” aliongeza Ndugu Moshingi.

Akizungumza kuhusu matarajio ya uwekezaji katika reli ya kisasa wakati ambapo kipande cha Dar es Salaam kikielekea kukamilika, Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji TRC Bi. Nzeyimana Dyegula amesema kuwa mbali na wadau wa kifedha, wadau kutoka sekta mbalimbali zinazogusa biashara pia wanayo fursa katika mradi.

“Tunawahimiza wadau wengine kuja kuona uwekezaji mkubwa wa serikali katika mradi huu wa kimkakati waangalie sehemu nyingine za uwekezaji, tuna ujenzi wa maeneo ya kuhifadhia makasha, karakana na maeneo mengine mbalimbali yatakayochochea shughuli za kiuchumi kando ya reli hii” alisema Bi. Nzeyimana.

Mradi wa Ujenzi wa reli ya kisasa unaotekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa awamu ya kwanza kati ya Dar es Salaam na Mwanza (km 1219) mpaka sasa unaendelea vizuri katika vipande vya Dar es Salaam – Morogoro (93%), Morogoro Makutupora (70%) na kipande cha Mwanza – Isaka kilichopo katika hatua za mwanzo za ujenzi.

# NSSF YAFURAHISHWA NA WAKANDARASI WA SGR KWA KUWASILISHA MICHANGO YA WAFANYAKAZI

Na Mwandishi wetu



*Meneja Mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Morogoro - Makutupora Mhandisi Mateshi Tito akiwapatia maelezo wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii - NSSF kuhusu maendeleo ya mradi wa SGR katika ukumbi wa mikutano uliopo kambi ya SGR Kilosa mkoani Morogoro, Septemba 2021.*



*Meneja Mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Morogoro - Makutupora Mhandisi Mateshi Tito akiwaelezea wajumbe wa Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii - NSSF kuhusu ubora wa mataruma na reli zilizotumika katika ujenzi wa reli mpya ya kisasa katika Mahandaki Kilosa mkoani Morogoro walipofanya ziara kuona mradi huo, Septemba 2021.*

Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii – NSSF watembelea mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR kipande cha pili Morogoro – Makutupora kwa lengo la kujifunza na kuona maendeleao ya mradi huo hivi karibuni, Septemba 2021.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wafadhili ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii Balozi Ali Iddi Siwa ameeleza lengo la ziara hiyo

"Tumekuja kutembelea mradi huu wa SGR kujua kinachoendelea kwa sababu NSSF ni mdau mkubwa wa maendeleo hapa nchini lakini jukumu letu ni kuvuna wanachama na mradi huu unajengwa na kampuni binafsi na wafanyakazi wa kampuni hii ni wanachama wetu" alisema Balozi Ali

Balozi Ali ameongeza kuwa "Tunashukuru kwamba Kampuni hizi zinatimiza masharti yote ya NSSF na tunakusanya michango, lakini pia reli hii inakwenda kuinua kazi za vikundi na kuzalisha njia nyingine za kujenga uchumi kupitia hilo linakwenda kutupatia wanachama zaidi"

Mkurugenzi Mkuu NSSF Bwana Masha Mshomba ameipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na serikali nyingine zilizopita kwa utekelezaji wa mradi wa SGR kwa sababu kwa namna moja au nyingine zilihusika katika kazi hiyo.

Mkurugenzi Mkuu amesema kuwa "Kwetu NSSF mradi huu ni muhimu sana kwa sababu umetoa ajira na jukumu letu ni kuwafikia watu wote ikiwemo sekta binafsi na Mhe. Rais Samia alituelekeza kuwa tuwafikie wote katika sekta binafsi pamoja na wale ambao hawako katika sekta rasmi, hivyo tunao wajibu wa kujiridhisha kuwa tunawafikia wote wanaofanya kazi katika mradi huu, lakini pia tutahakikisha wote wanaokuja kufanya kazi katika mradi huu wanapata hifadhi ya jamii" alisema Bwana Masha

Meneja Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR Morogoro – Makutupora Mhandisi Mateshi Tito amesema kuwa NSSF ni wadau wakubwa kwa TRC pamoja miradi yake kwa sababu ina wafanyakazi na watumishi ambao ni wanachama na wamekuwa wakishirikiana katika masuala mbalimbali yanayohusu hifadhi za watumishi.

"Ujio wa NSSF ni neema kwa sababu mradi wetu umetoa ajira kwa watu zaidi ya 13,000 ambao wote ni wanachama wa NSSF hivyo ujio wao ni sehemu ya kuwatembelea wanachama wake na kujenga mahusiano ya wanachama na NSSF" alisema Mhandisi Mateshi

Mhandisi Mateshi aliongeza kuwa wajumbe wa Bodi ya Wadhamini NSSF wamejiridhisha kwa kuwa michango ya wanachama wao inapelekwa kwa wakati lakini pia NSSF ni wadau katika kuwezesha utekelezaji wa miradi kwa kuweka fedha ili kuunga mkono jitihada za serikali katika kiutekeleza miradi ya kimkakati ukiwemo mradi wa SGR.

# FIDIA ZA MAENEO YA NYONGEZA ZAWANUFAISHA WANANCHI MOROGORO NA DODOMA

Na Mwandishi wetu



Afisa wa masuala ya kijamii Bi. Catherine Mwakagali akimsajili Bi. josephine Suda, mkazi wa mtaa wa Image katika orodha ya wananchi waliopatiwa fidia mkoani Dodoma, hivi karibuni Septemba 2021.

Shirika la Reli Tanzania – TRC limeendelea na zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa ili kupisha shughuli za mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR ikiwa ni maeneo ya nyongeza kwa kipande cha Morogoro – Makutupora ambacho ujenzi wake umefika zaidi ya asilimia 73, Septemba 2021.

Zoezi limeendeshwa na maafisa kutoka TRC pamoja na viongozi na maafisa watendaji wa maeneo husika ya mkoa wa Morogoro ambayo ni Kikundi, Kimambila, Mkwatani, Mkadage, Mwasa pamoja na mkoa wa Dodoma katika maeneo ya Igandu, Chilwana, Zuzu, Kigwe, Miganga, Bahi Nakulu, Bahi Sokoni na Bahi Mapinduzi.

Mtendaji wa kijiji cha Igandu mkoani Dodoma Bwana Jonalis Kibendera ameeleza kuwa wananchi wamekuwa na wasiwasi kwamba huenda malipo yangechelewa lakini ameishukuru Serikali kwa kufanikisha zoezi hilo na kuwapatia wananchi fidia ambazo zinakwenda kubadilisha maisha yao.

“Walikuwa na wasiwasi kwamba malipo haya yangechelewa, lakini naishukuru serikali, kwahiyo fedha hizi zitawasaidia kuleta maendeleo pia naushukuru mradi ambao umepita katika kijiji changu kwa sababu Stesheni hii (Igandu) itawasaidia kusafirisha mazao yao na kwenda kununua bidhaa kwa urahisi na kurudi kwa urahisi” alisema Bwana Jonalis.

Wilson Yona ni mmoja wa wananchi ambao wamepokea fidia katika kijiji cha Igandu mkoani Dodoma ambapo emeeleza faida za mradi na kuishukuru serikali kwa kuwapatia fidia na vifuta machozi ili kupisha ujenzi wa miundombinu ya reli ya kisasa
“Naishukuru Serikali nimepata fidia, mradi huu umewanufaisha watu wengi, vijana wengi wapo kwenye mradi huu na wengi wamefanikiwa kujenga nyumba kupitia mradi huu, tunaushukuru mradi huu na tunaishukuru Serikali pia” alisema Bwana Yona

Mwantumu Shabani, mkazi wa Zuzu mkoani Dodoma amesema kuwa “Eneo langu mara ya kwanza limechukuliwa na likalipwa na limechukuliwa mara ya pili na nimelipwa, mradi huu utasaidia kutupunguzia muda wa safari na kurahishisha shughuli za kibiashara”

Maeneo ya nyongeza hutwaliwa kwa ajili ya shughuli za ziada za mkandarasi ambazo hazihusishi ujenzi wa tuta la reli ambalo kwa kiasi kikubwa eneo lake liko tayari kwa ajili ya ujenzi na tayari ujenzi unaendelea.

Na Mpiga Picha wetu



Timu ya TCB na menejimenti ya TRC wakishuhudia moja ya hatua za zoezi la uchomeaji reli kwa teknolojia ya *'Flash Butt Welding'*, umbali wa km 274 kutoka Dar es Salaam, Kilosa mkoani Morogoro, Septemba 2021.



Meneja mradi wa SGR Moro - Makutupora, Mhandisi Mateshi Tito (mwenye Kofia) akimuelezea Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya TCB Sabasaba Moshingi (Katikati) maendeleo ya Ujenzi wa stesheni ya SGR Kilosa mkoani Morogoro, Septemba 2021.



Timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango wakipata maelezo kutoka kwa Meneja Msaidizi Mradi wa SGR Morogoro - Makutupora Mhandisi Christopher Mang'wela (aliyevaa miwani) kuhusu maendeleo ya mradi huo katika eneo la Kimambila mkoani Morogoro, Septemba 2021.



Wataalamu kutoka Wizara ya Fedha na Mipango wakiwa katika picha ya pamoja na Meneja Msaidizi Mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR Dar es Salaam - Morogoro Mhandisi Thadei Paul (kulia) katika kituo cha umeme wa SGR Kingolwira mkoani Morogoro, Septemba 2021.




Muonekano wa nje wa jengo la Stesheni ya reli ya kisasa - SGR Kilosa mkoani Morogoro likiwa limekamilika.



Muonekano wa ndani wa jengo la Stesheni ya reli ya kisasa - SGR Kilosa mkoani Morogoro likiwa limekamilika.



## Mhe. Kassim Majaliwa
**Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Nimeanza kukagua njia kutoka jijini Dar es Salaam hadi Kilosa kwa upande wa vituo vimekamilika na mimi nimejionea, reli hii ya kimkakati imejengwa kwa kiwango inachoridhisha. Nilikuwa naangalia maeneo ya vivuko vya binadamu na wanyama na yote yamezingatiwa na mkoa wenu wa Morogoro ndiyo vipo vingi

Tunachosubiri ni behewa zetu ambazo yanakuja mwezi wa 11 ili waanze kuziweka na kuunganisha na umeme ili zianze kutembea na huduma zianze kufanyika, hatua ya awali baada ya behewa kuja mwezi wa 11 tutaanza na uendeshaji wa Dar es salaam na Morogoro

Leo hii natembea kwenye reli kuanzia Pugu mpaka Kilosa maana yake ujenzi wa reli sasa unaelekea kukamilika, kwahiyo watanzania muendelee kuwa na imani ya kuwa ujenzi wa reli unaendelea, ujenzi wa reli unasimamiwa, na ujenzi wa reli utakamilika



Tunaamini kazi hii itakamilika, ni wajibu wetu sisi tunaomsaidia Mhe. Rais kupita kwenye miradi hii kufuatilia na kuwahabarisha watanzania hatua iliyofikiwa, tunajua kuna watanzania tunao hapa tunaamini ukamilishaji wa hili unatokana na kasi yenu, huu ni mradi wetu kwahiyo muendelee kufanya kazi kwa nguuvu zote ili mradi ukamilike

## Mhe. Kassim Majaliwa
**Waziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

## TRC NA YAPI MERKEZI WATOA MSAADA



Bwana Silasi Kasao, mkazi wa Kimamba mkoani Morogoro akionesha makabrasha ya Bajaji aliyokabidhiwa na TRC alipowasili ofisi ya TRC jijini Dar es Salaam, Septemba 2021.

Na Mwandishi wetu

Shirika la Reli Tanzania - TRC kwa kushirikiana na Mkandarasi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR kampuni ya YAPI MARKEZI limempatia bajaji yenye thamani ya Shilingi milioni 8 Bw. Silasi R. Kasao mkazi wa Kijiji cha kimamba, Kilosa Mkoani Morogoro, ikiwa ni msaada wa kutatua changamoto za usafiri na kumsaidia katika kuongeza kipato.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu TRC Ndugu Masanja kadogosa ameamua kugharamia masomo yake ya chuo kikuu kwa miaka 3, ambapo Bwana Silasi anatarajia kuanza masomo ya shahada ya sheria mwezi, Oktoba 2021 katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Tumaini Dar es Salaam (TUDARCo).

## TRC YAKABIDHI ENEO KWA MKANDARASI



Moja kati ya eneo ambalo mkandarasi amekabishidhiwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa njia ya reli ya kisasa Mwanza - Isaka katika kijiji cha Seke Bugoro mkoani Simiyu, Septemba 2021.

Shirika la Reli Tanzania – TRC lakabidhi eneo lenye jumla ya urefu wa KM 30 kwa mkandarasi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha tano Mwanza – Isaka (km 341) katika maeneo ya Seke Bugoro (km 1), Nyashimba (km 5), Muhida (km 7), Bukigi (km 4) na Lali (km 3), Bokene na Lishololo (km 10).

Kipande cha eneo katika kijiji cha Seke Bugoro wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga chenye urefu wa km 1 tayari kimesafishwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa njia ya reli huku vipande vingine vikiwa katika maandalizi ya kusafishwa kwa ajili ya ujenzi.

TRC inaendelea na taratibu za kuhakikisha mkandarasi anapata maeneo kwa wakati ili aweze kuanza kazi ikiwemo kukamilisha zoezi la uthamini na kulipa fidia za maeneo ambayo mradi huo utapita.

## KADOGOSA ATOA WITO KWA HALMASHAURI KUISEMEA MIRADI YA KIMKAKATI

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania, Masanja Kadogosa ameshiriki na kuwasilisha mada ya maendeleo ya ujenzi wa reli ya kisasa - SGR, katika mkutano mkuu maalumu wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) Ukumbi wa Mikutano wa J.M Kikwete Dodoma, Septemba 2021.

Pamoja na mambo mengine, Kadogosa ameeleza kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan inatekeleza kwa kasi kubwa miradi ya Kimkakati ukiwemo mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa SGR hivyo kuna kila sababu ya kuisemea na kuitangaza miradi hiyo.

“Huu ni Mradi (SGR) wa wananchi kwahiyo lazima watambue una faida gani kwao, wakielezwa kwa lugha nyepesi itasaidia kuelewa lengo la Serikali, na kubwa zaidi ni kumsaidia Mhe. Rais ambaye anafanya kazi kubwa sana katika kutekeleza miradi hii”



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa, akizungumza wakati akiwasilisha mada juu ya Mradi wa Ujenzi wa SGR wakati wa Mkutano Mkuu maalum wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania, jijini Dodoma

# ATHARI ZA KUTOFUATA ULINZI NA USALAMA WA RELI

Na Mwandishi wetu


Usafiri wa reli ni miongoni mwa njia ya usafirishaji unaoaminika kwa kuzingatia usalama zaidi duniani kote kwa ajili ya usafirishaji wa abiria na mizigo.

Shirika la Reli Tanzania - TRC kwa kupitia Sheria namba 10 ya reli ya mwaka 2017, TRC imepewa dhamana ya kuhakikisha inasimamia vyema usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kuzingatia usalama, vilevile Shirika limepewa dhamana ya kusimamia ujenzi na maendeleo mbalimbali ya miradi na miundombinu ya reli nchini.

Kutokana na majukumu hayo ya Shirika la Reli Tanzania suala la kuhakikisha sera zinazohusiana na usalama wa abiria, mizigo na miundombinu ya reli zinatungwa na kufuatiliwa ipasavyo ni moja ya mambo ya msingi ambayo Shirika linazingatia kabla ya kuendesha shughuli za usafirishaji.

TRC ina kitengo maalumu ambacho kinasimamia na kushughulikia ulinzi na usalama wa miundombinu ya reli, abiria na mizigo pia kupitia kitengo hicho imeainisha baadhi ya mienendo au shughuli ambazo kwa namna moja au nyingine zinachagiza kuhatarisha usalama wa abiria, miundombinu ya reli pamoja na mizigo kama ifuatavyo; kukatiza vivuko bila tahadhari, kuweka vitu vizito kwenye reli, uharibifu wa mazingira yanayozunguka miundombinu ya reli, kutozingatia matumizi sahihi ya alama za usalama wa reli, kuvusha mifugo maeneo yasiyo rasmi pamoja na shughuli za kibinadamu kandokando ya reli.

## RAMANI YA MAELEKEZO YA MATUMIZI YA MAKUTANO YA RELI NA BARABARA




Kutokana na sababu hizo suala la usalama wa reli limekumbwa na changamoto nyingi ambapo zisipotatuliwa zinaweza kuleta athari kwa jamii.

Miongoni mwa athari hizo ni vifo na majerehi kwa wahusika, ni dhahiri kwamba pindi itokeapo ajali huleta athari kubwa ikiwemo vifo na majeruhi na kuwapoteza wapendwa wetu na nguvukazi ya taifa.


Pili ni uharibifu wa miundombinu ya reli, ajali inapotekea miundombinu ya reli huharibika kutokana na kuanguka kwa behewa au kishindo unaosababishwa na ajali hiyo na kupelekea behewa kuharibika, reli kung'oka, majengo pamoja na mali zilizopo karibu kuharibiwa kutokana na ajali.

Tatu, gharama za matengenezo ya njia ya reli pamoja na behewa, inapotekea ajali kwa ajili ya kutofuata sheria za usalama wa reli ni kubwa na ni hasara kwa Shirika na taifa, miundombinu ya reli inapoharibika kutokana na ajali Shirika hulazimika kuhakikisha hali ya miundombinu hiyo inarudi katika ubora wake ili kuruhusu shughuli za usafiri kuendelea kama kawaida, sambamba na miundombinu behewa zilizoharibika hufanyiwa ukarabati ili kukidhi mahitaji ya huduma.

Mwisho athari zitokanazo na kutofuata uslama wa reli ni upotevu wa muda mwingi katika kuokoa majeruhi, mali, mizigo na ukarabati wa behewa na miundombinu ya reli illiyoharibika, muda huu ungetumika katika kufanya shughuli nyingine za uzalishali na kuleta mendeleo yakinifu kwa Shirika pamoja na nchi kwa ujumla.

Kutokana na athari hizo kuna ulazima wa kila mwananchi kuchukua hatua madhubuti kwa nafasi yake ili kuokoa maisha ya watu, kuokoa mali na miundombinu ya reli, Shirika lina namba ya bure (0800110042) ambayo mwananchi anaweza kupiga na kuripoti hujuma katika miundombinu ya reli.

Aidha, Shirika la Reli Tanzania, kupitia kitengo chake cha Ulinzi na Usalama wa Miundombinu ya Reli limekuwa likitoa elimu kwa jamii kuainisha matumizi sahihi ya alama za usalama wa reli ikiwemo kuangalia pande zote mbili kabla ya kuvuka reli,kama hakuna treni vuka kivuko cha reli kwa muda usiozidi sekunde tatu na kufuata maelekezo kutoka kwa afisa wa usalama barabarani



**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**
**Barabara ya Sokoine**
**S.L.P 76959**
**Dar es Salaam**
**TANZANIA**
**Barua pepe; info@trc.co.tz**
**Simu ya Bure; 0800 110 042**

**Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano**
**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**

| | |
|---|---|
| **MHARIRI MKUU** | **Jamila Mbarouk** |
| **MHARIRI MSAIDIZI** | **Sami Omary** |
| **MAKALA** | **Aziza Charles & Hemed Mohamed** |
| **HABARI** | **Amina Juma** |
| **PICHA** | **Seleman Kadiko Hassan Said** |
| **MTAYARISHAJI** | **Sami Omary** |

**tzrailways TRC Reli TV www.trc.co.tz**

**Reli Yetu | Maendeleo Yetu | Taifa Letu #TRCMpya**